JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA

9 JULAI, 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA – TAREHE 9 JULAI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:

Taarifa ya Majumuisho ya Mpango Mkakati wa Kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Wizara, Idara za Serikali na Mikoa kwa Mwaka wa Fedha, 2008/2009.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

191. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Barabara ya kutoka kijiji cha Makutupa hadi kijiji cha Bumila Wilayani Mpwapwa inahitaji matengenezo makubwa ili iweze kupitika wakati wote lakini lipo korongo kubwa karibu na shule ya Msingi Bumila ambalo hufanya wananchi pamoja na wanafunzi kushindwa kuvuka kwenda shule kutokana na maji kujaa wakati wa mvua:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara hiyo inatengenezwa na kujenga daraja katika korongo hilo ili kuondoa adha hiyo kwa wananchi wa Bumila.

192. MHESHIMIWA BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA (LUSHOTO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kusaidia ujenzi wa zahanati za vijiji zinazojengwa kwa nguvu za wananchi zikiwemo zahanati za vijiji vya Miegeo, Ngulwi, Kwemashai, Mazumbai, Mavului, Ungo, Mbelei, Mdando, Bombo na Irente Wilayani Lushoto.

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

193. MHESHIMIWA SAID AMOUR ARFI (MPANDA KATI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Benki kama **NBC, STANBIC,**

Standard Charted na **CRDB** zina wateja wenye majina na vipato vikubwa na nyingine zilianzishwa kwa lengo la kutoa huduma katika miji mikubwa tu:-

Je, Serikali iko tayari kusaidia juhudi za kushawishi Benki ambazo bado Watanzania wana kauli (mfano **CRDB** na Posta) kufungua matawi na kutoa huduma katika Mji wa Mpanda ambao una tawi la **NMB** pekee na halikidhi mahitaji ya wananchi wakati huu wa ushindani.

194. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Kumekuwepo na ugumu wa kuwakopesha wafugaji na wakusanyaji matunda chini ya mpango wa Taifa wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, kwa sababu ya kuwa na elimu duni ya darasani, na uelewa mdogo wa jambo hilo hivyo kushindwa hata kubuni miradi ya biashara za kufanya baada ya kuchukua mikopo:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya makusudi ya kusaidia jamii hizo ambazo ndio hasa walengwa ili nao wafaidi mpango huo wa kuwawezesha wananchi kiuchumi;

(b) Je, hadi sasa ni **SACCOS** ngapi zilizokopesha fedha hizo Basotu – Hanang, Orkesment huko Simanjiro na Yaeda Chini huko Mbulu, na ni watu wangapi wamenufaika.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:

195. MHESHIMIWA MOHAMED HAMIS MISSANGA (SINGIDA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko:- Ajali za barabarani zinaendelea kuongezeka siku hadi siku, na ajali nyingi kati ya hizo zinasababishwa na upasukaji wa mipira hasa ya mbele ya magari husika:-

(a) Je, Kwa nini Serikali inaruhusu kuingizwa nchini tairi zisizo na viwango vya ubora ambazo

zinachangia kuongezeka kwa ajali za barabarani hasa kwa mabasi na malori;

(b) Kiwanda cha Matairi cha General Tyre – Arusha kilikuwa kikizalisha Matairi yenye viwango vya ubora; Je, ni sababu zipi zilifanya kiwanda hicho kufungwa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

196. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBASWA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kituo cha Polisi cha Lupa kinahudumia Tarafa nzima ya Kipambawe yenye Kata saba lakini hakina usafiri kabisa hali inayohatarisha ulinzi na usalama:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari kituoni hapo.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

197. MHESHIMIWA PINDI HAZARA CHANA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Serikali ina mpango wa kuboresha Kilimo cha Kisasa ambacho ndiyo msingi wa Uchumi wa Kisasa:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuanzisha bwawa la umwagiliaji na shughuli zingine kama ufugaji wa Samaki katika eneo la Ipogolo Mkoani Iringa sehemu ambayo maji hutuama sana;

(b) Je, Serikali ina mpango wa kuanzisha miradi ya umwagiliaji na mabwawa

katika Wilaya ya Ludewa na Makete ambako kuna vyanzo vingi vya maji yanayofaa kwa umwagiliaji na ufugaji wa Samaki.

198. MHESHIMIWA DKT. IBRAHIM SAID MSABAHA (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Katika Mradi wa Maji wa Wami - Chalinze, Serikali iliahidi kufikisha maji kwa awamu katika vijiji vya Gwata, Gumba na Magindu katika Wilaya ya Kibaha lakini hadi sasa ahadi hiyo haijatekelezwa:-

Je, ni lini wananchi wa vijiji hivyo wategemee kupata maji ya bomba.

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

199. MHESHIMIWA RUTH BLASIO MSAFIRI (MULEBA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Hospitali za kujitolewa hasa zinazoendeshwa na Mashirika ya Dini zinatoa mchango mkubwa sana katika kutoa huduma nzuri tangu tupate uhuru lakini bado zinahitajika katika baadhi ya maeneo kama vile Jimbo la Muleba Kaskazini:-

Je, Sekalini ina utaratibu gani wa kuzisaidia hospitali hizo ili huduma hiyo isitetereke na kusababisha baadhi ya watumishi wengi kuhamia Serikalini.

200. MHESHIMIWA MCH. DK. GERTRUDE RWAKATARE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- **MEWATA** wanatoa huduma nzuri sana ya kuwasaidia wanawake wenye saratani ya matiti na kwa huduma yao wameokoa mamilioni ya pesa na maisha ya wanawake wengi; lakini Madaktari hao inabidi wachangiwe

kupitia kwenye televisheni kama ombaomba:-

Je, kwa nini Serikali isitenge fungu maalum la fedha kwa kazi hiyo muhimu wanayoifanya.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

DODOMA
9 JULAI, 2010

DKT. T.D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE